MERIT

# UBASHIRI WA KCPE TARGETER
## DARASA LA NANE - 2022

1

## KISWAHILI:
## SEHEMU YA KWANZA:
## LUGHA

**Muda: Saa 1 Dakika 40.**

UBASHIRI WA KWANZA WA KCPE

### MAAGIZO KWA WATAHINIWA
### SOMA MAAGIZO YAFUATAYO KWA MAKINI.

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibu. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu, andika katika kijitabu hiki.
3. Ukiisha kuchagua jibu lako, lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala **sio** katika kijitabu cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU.**

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba umeandika yafuatayo katika karatasi ya majibu:

**NAMBARI YAKO YA MTIHANI**
**JINA LAKO**
**JINA LA SHULE YAKO**

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani nambari ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu, na usiikunje.
9. Kwa kila swali **1-50,** umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi **A, B, C, D**. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

**Mfano**

**Katika kijitabu cha maswali: Chagua jibu sahihi.**

18. Chagua sentensi iliyotumia -na- kuonyesha hali.
    A. Ng'ombe walipelekwa malishoni na mchungaji.
    B. Jaidi na Salima walisoma kwa bidii.
    C. Tuliingiwa na hofu gari lilipokosa mwelekeo.
    D. Mkulima ananyunyizia mimea maji.

Jibu sahihi ni **C**

Katika karatasi ya majibu

**16.** [A] [B] [C] [D] **17.** [A] [B] [C] [D] **18.** [A] [B] [C] [D] **19.** [A] [B] [C] [D]

**18,** kisanduku chenye herufi **C** ndicho kilichochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku **kimoja** tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kijitabu hiki cha maswali kina kurasa 8 zilizopigwa chapa.**

*Huchapishwa na kuratibiwa na taasisi ya uchapishaji ya Targeter Educational Publishers Ltd.*
*Email: info@targeterpublishers.co.ke*

**GEUZA UKURASA**

Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | **Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.***

Hakuna mtu yeyote yule anayeweza kuishi peke yake __1__ kutangamana na wengine. Kama __2__ waswahili, __3__. Ni vigumu sana kwa jamii __4__ kuendelea bila ushirikiano wa kila mmoja. __5__ mwanafunzi anapokuwa shuleni __6__ kushirikiana na wenzake katika shughuli __7__ za shuleni.

1. A. pasi na B. pasi ya C. nje ya D. juu ya
2. A. waliosema B. walisema C. waliyosema D. walivyosema
3. A. ukiona vyaelea jua vimeundwa
   B. jitihanda haiondoi kudura
   C. ukuni mmoja hauwaki moto
   D. manahodha wengi chombo huenda mrama
4. A. wowote wale B. lolote lile C. yoyote ile D. wowote ile
5. A. Maadamu B. Mathalani C. Madhali D. Mithili
6. A. ana budi B. hawezi C. ilimbidi D. hana budi
7. A. anuwai B. shelabela C. kichele D. anwani

__8__ shughuli hizi za shuleni ni ufunzaji wa lugha. Kumbuka mtu __9__ lugha huanza kwa __10__ za lugha hiyo. Hata katika utamkaji ushirikiano wa __11__ lazima uwepo. Kumbuka sauti hizi huundwa kwa silabi. Kwa mfano neno 'kilichowashughulisha' lina silabi __12__. Kando na silabi mwanafunzi pia hujifunza viambishi vya aina mbalimbali. kwa mfano 'wa' katika 'aliwapenda' inaonyesha '__13__'. Kwa ufupi ushirikiano ni mzuri na mwanafunzi __14__ hivyo, huenda __15__ katika jitihada zake za kutafuta ufanisi wa kielimu.

8. A. Baadhi ya B. Miongoni mwa C. Pamoja na D. Nje ya
9. A. asipojifunza B. asiyofanya C. anapojifunza D. angalifanya
10. A. kusoma sauti B. kuona herufi C. kutamka sauti D. kuelezea sauti
11. A. chanda na pete B. lijamu na hatamu C. gidamu na njuti D. sweta na shati
12. A. 20 B. 16 C. 12 D. 8
13. A. kitenzi B. wakati C. watendewa D. watenda
14. A. asipofanya B. asifanye C. asingefanya D. akifanya
15. A. akalia n'goa B. akapiga vijembe
    C. akaambulia patupu D. akatia mbugi mguuni

**Kutoka swali la 16 mpaka 30, chagua jibu sahihi.**

16. **Andika katika usemi halisi:**
*Kaka aliniambia kuwa tungeenda shambani siku ambayo ingefuata.*
A. "Utaenda shambani kesho," Kaka aliniambia.
B. "Kesho wanaenda shambani," kaka aliniambia.
C. "Tungeenda shambani kesho," kaka aliniambia.
D. "Mtaenda shambani kesho," kaka aliniambia.

17. Orodha gani ina nomino za ngeli ya U - YA pekee?
A. Upishi, uwele, ulezi
B. Ubaya, utiifu, ugonjwa
C. Mabele, mabua, machozi
D. Mazingira, manukato, maziwa

18. **Maana ya methali:**
*'Ganda la muwa la jana chungu kaona kivuno.'* ni
A. Jambo ambalo unaliona rahisi kwako kwa mwenzako huenda likawa gumu.
B. Haifai kudharau kitu chako duni kwa kutamani cha mwenzako.
C. Haifai kuwadharau watu waliokusaidia hapo awali huenda ukawahitaji baadaye.
D. Kitu unachokiona duni kwako, huenda kikawa na manufaa kwa mtu mwingine

19. **Chagua ukanusho ufaao zaidi wa:**
*Zuhura alikuwa akiwapokea na kuwakaribisha wageni.*
A. Zuhura hakuwa akiwapokea na kuwakaribisha wageni.
B. Zuhura hakuwa akiwapokea wala kuwakaribisha wageni
C. Zuhura alikuwa hapokei ila kuwakaribisha wageni.
D. Zuhura alikuwa hapokei bali kuwakaribisha wageni

20. Sentensi iliyo na 'na' ya nafsi ni ipi?
A. Wakulima wanapalilia mimea yao
B. Mimi nina mafua makali
C. Mtaro ulichimbwa na wavulana wale
D. Naona vyema tuianze kazi hii

21. **Andika wingi wa sentensi ifuatayo:**
*Sogora aliondoka jukwaani wimbo ulipokamilika*
A. Sogora waliondoka jukwani wimbo ,ulipokamilika
B. Masogora waliondoka jukwaani wimbo ulipokamilika
C. Masogora waliondoka majukwaani nyimbo zilipokamilika.
D. Sogora waliondoka majukwaani nyimbo zilipokamilika

22. **Ni ipi kauli ya kutendea ya sentensi ifuatayo:**
*Seremala alienda kiwandani akatengeneza meza.*
A. Kiwandani walitengenezea seremala meza.
B. Meza ilitengenezwa kiwandani na seremala
C. Seremala alitengenezea meza kiwandani
D. Seremala alitengenezewa meza kiwandani.

23. **Ainisha maneno yaliyoangaziwa katika sentensi ifuatayo:**
*Mwanafunzi* ***mtiifu aghalabu*** *huwapendeza walimu wake.*
A. Kiwakilishi, kiunganishi
B. Kivumishi, kihusishi
C. Kivumishi, kielezi
D. Kiwakilishi, kielezi

24. **Tambua kiwakilishi katika sentensi ifuatayo:**
*Wake mdogo alijiunga na shule hii juzi:*
A. Juzi
B. Wake
C. Mdogo
D. alijiunga

**25. Kiambishi -ki- kimetumika vipi katika sentensi ifuatayo:**

*Wanafunzi wale walikuwa wakizingatia nidhamu.*

A. Kuonyesha masharti.
B. Kuonyesha jinsi ya kuendelea
C. Kuonyesha jinsi ya kutenda
D. Kuonyesha vitendo vinavyofanyika pamoja.

**26. Akifisha sentensi ifuatayo kwa usahihi:**

*Mwalimu aliwauliza mnafanya nini hapa.*

A. Mwalimu alitaka kujua walichokuwa wakifanya hapo?
B. Mwalimu aliwauliza, "Mnafanya nini hapa?"
C. Mwalimu aliwauliza, "mnafanya nini hapa?"
D. Mwalimu aliwauliza, "Mnafanya nini hapo?"

**27. Unganisha sentensi zifuatazo kwa usahihi:-**

*(i) Mwanafunzi alifanya vyema*
*(ii) Mwanafunzi alijitahidi sana*

A. Mwanafunzi alifanya vyema na kujitahidi sana
B. Mwanafunzi alijitahidi sana akafanya vyema
C. Mwanafunzi alifanya vyema ingawa alijitahidi sana
D. Mwanafunzi alijitahidi sana ila hakufanya vyema.

**28.** Chagua sentensi yenye kiwakilishi cha idadi.

A. Mwanafunzi aliyefika kwanza alimpata mwalimu wa pili darasani.
B. Mwalimu aliyetufunza mwanzoni alituuliza swali moja mara mbili.
C. Mwalimu aliyetufunza mwanzoni alitufafanulia mambo kadha ya kutufaa
D. Mwanafunzi aliyefika kwanza alipewa medali na wa pili akapewa kitabu.

**29.** Maneno yafuatayo yatafuatana vipi katika kamusi?

*(i) Mchuuzi* *(ii) Mchumba*
*(iii) Muhogo* *(iv) Muhina*

A. (ii), (i), (iv), (iii) B. (iv), (iii), (ii), (i)
C. (ii), (i), (iv), (iii) D. (i), (ii), (iv), (iii)

**30.** Ni jibu lipi lenye nomino iliyoundwa kutokana na kitenzi?

A. Nyweka - nywesha
B. Ogopa - ogofya
C. Saka - usasi
D. Amini - aminifu

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 mpaka 40.**

Ukiwauliza watu kwa nini wanaishi eneo fulani na si jingine, sababu anuwai zitatolewa. Kuna wale watatoa sababu za kuzumbua riziki. Wengine watasema ni juu ya usalama wao. Hawa wa usalama, wanakaa hapo kwa sababu ya amani. Amani ni hali inayofaa kuenziwa na kuimarishwa kila wakati na kila mahali. Baadhi ya watu huamini kuwa amani haipatikani ila kwa ncha ya upanga lakini si kweli wakati wote. Amani ya kudumu huweza pia kupatikana kwa njia ya maafikiano.

Ukosefu wa amani una gharama kubwa isiyolipika kwa urahisi. Wahenga waliosema, **'kama hujui kufa tazama kaburi,'** hawakukosea. Tulitaka kuyajua maafa yaletwayo na vita katika ukanda huu wa Afrika Mashariki, tuna mifano kem kem. Si nchini, si majirani, twaweza kujifunza mengi kuhusu umuhimu wa amani na hasara zinazoletwa na kinyume chake.

Kwa ufupi amani ni hali ya utulivu ambayo hupatikana pasipo na vita wala machafuko yoyote. Mara nyingi hali hii hupatikana pasipo na gharama yeyote. Hili hasa ndilo linalowafanya wengi kutotilia maanani umuhimu wa amani. Lakini kama nilivyokudokezea hapo awali asiyejua thamani ya mwangaza aingie gizani. ushahidi kuhusu matokeo ya ukosefu wa amani nirudie tena umeenea vururu katika janibu nyingi.

Yumkini kama si yamkini nilikuuliza kama unajua umuhimu wa amani utakuwa mwepesi wa kukubali. Hata hivyo ukituama na kuwazia matukio mbalimbali yaliyowahi kutokea karibu nawe, au hata kwa mchango



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi **| Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

**25.** **Kiambishi -ki- kimetumika vipi katika sentensi ifuatayo:**
*Wanafunzi wale walikuwa wakizingatia nidhamu.*
A. Kuonyesha masharti.
B. Kuonyesha jinsi ya kuendelea
C. Kuonyesha jinsi ya kutenda
D. Kuonyesha vitendo vinavyofanyika pamoja.

**26.** **Akifisha sentensi ifuatayo kwa usahihi:**
*Mwalimu aliwauliza mnafanya nini hapa.*
A. Mwalimu alitaka kujua walichokuwa wakifanya hapo?
B. Mwalimu aliwauliza, "Mnafanya nini hapa?"
C. Mwalimu aliwauliza, "mnafanya nini hapa?"
D. Mwalimu aliwauliza, "Mnafanya nini hapo?"

**27.** **Unganisha sentensi zifuatazo kwa usahihi:-**
*(i) Mwanafunzi alifanya vyema*
*(ii) Mwanafunzi alijitahidi sana*
A. Mwanafunzi alifanya vyema na kujitahidi sana
B. Mwanafunzi alijitahidi sana akafanya vyema
C. Mwanafunzi alifanya vyema ingawa alijitahidi sana
D. Mwanafunzi alijitahidi sana ila hakufanya vyema.

**28.** Chagua sentensi yenye kiwakilishi cha idadi.
A. Mwanafunzi aliyefika kwanza alimpata mwalimu wa pili darasani.
B. Mwalimu aliyetufunza mwanzoni alituuliza swali moja mara mbili.
C. Mwalimu aliyetufunza mwanzoni alitufafanulia mambo kadha ya kutufaa
D. Mwanafunzi aliyefika kwanza alipewa medali na wa pili akapewa kitabu.

**29.** Maneno yafuatayo yatafuatana vipi katika kamusi?
*(i) Mchuuzi* *(ii) Mchumba*
*(iii) Muhogo* *(iv) Muhina*
A. (ii), (i), (iv), (iii) B. (iv), (iii), (ii), (i)
C. (ii), (i), (iv), (iii) D. (i), (ii), (iv), (iii)

**30.** Ni jibu lipi lenye nomino iliyoundwa kutokana na kitenzi?
A. Nyweka - nywesha
B. Ogopa - ogofya
C. Saka - usasi
D. Amini - aminifu

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 mpaka 40.***

Ukiwauliza watu kwa nini wanaishi eneo fulani na si jingine, sababu anuwai zitatolewa. Kuna wale watatoa sababu za kuzumbua riziki. Wengine watasema ni juu ya usalama wao. Hawa wa usalama, wanakaa hapo kwa sababu ya amani. Amani ni hali inayofaa kuenziwa na kuimarishwa kila wakati na kila mahali. Baadhi ya watu huamini kuwa amani haipatikani ila kwa ncha ya upanga lakini si kweli wakati wote. Amani ya kudumu huweza pia kupatikana kwa njia ya maafikiano.

Ukosefu wa amani una gharama kubwa isiyolipika kwa urahisi. Wahenga waliosema, **'kama hujui kufa tazama kaburi,'** hawakukosea. Tulitaka kuyajua maafa yaletwayo na vita katika ukanda huu wa Afrika Mashariki, tuna mifano kem kem. Si nchini, si majirani, twaweza kujifunza mengi kuhusu umuhimu wa amani na hasara zinazoletwa na kinyume chake.

Kwa ufupi amani ni hali ya utulivu ambayo hupatikana pasipo na vita wala machafuko yoyote. Mara nyingi hali hii hupatikana pasipo na gharama yeyote. Hili hasa ndilo linalowafanya wengi kutotilia maanani umuhimu wa amani. Lakini kama nilivyokudokezea hapo awali asiyejua thamani ya mwangaza aingie gizani. ushahidi kuhusu matokeo ya ukosefu wa amani nirudie tena umeenea vururu katika janibu nyingi.

Yumkini kama si yamkini nilikuuliza kama unajua umuhimu wa amani utakuwa mwepesi wa kukubali. Hata hivyo ukituama na kuwazia matukio mbalimbali yaliyowahi kutokea karibu nawe, au hata kwa mchango



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Mob: 0734579299
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

wako binafsi, utagundua kuwa umewahi kuchangia kuvuruga amani kwa njia moja au nyingine. Na mchango huu unaweza kutokea bila ya wewe kuwa na habari. Je, unakumbuka siku ambapo ulieneza uvumi kuhusu mwenzako darasani. Kwako najua ulichukulia tukio hilo kuwa la kawaida. Kile ambacho hukujua ni kuwa kwa kufanya hilo, ulimsababishia kutengwa na marafiki. Ulichangia unyanyapaa ukamfanya ajione duni na kumnyima amani. Kulonga mithaki ulimjeruhi sana kihisia. Elewa kuwa tabia ni kia cha mwili. Matendo ya aina hii **yasipothibitiwa** huweza kuwa msingi wa kusambaratisha mshikamano wa kitaifa baadaye.

Wengi wetu tunaamini kuwa vyombo vya dola vina jukumu la kudumisha amani. Hii ndiyo sababu watu wengi huinyoshea serikali kidole wakati yanapozuka machafuko yoyote nchini. Utawala uliopo hukashifiwa kwa kushindwa kutekeleza jukumu lake la kulinda raia wake. Hata hivyo watu wawa hawa ndio kwa mfano wanaowasetiri washukiwa serikalini kila wakati serikali inapojaribu kunyoosha mkono ili kuwafikia. Watu hawa wakiombwa na vyombo vya dola kutoa ushahidi utakaochangia kushtakiwa kwa washukiwa wenyewe wao hufyata ndimi zao. Aidha wanasiasa wachochezi hukimbilia kutafuta hifadhi za makabila yao pale wanapokabiliwa na mashtaka ya kuvuruga amani nchini. wao wakifisidi, walifanya hivyo kivyao lakini wakishikwa hao inakuwa mzigo wa jamii nzima. Hapa mjinga ni nani? Jibu lake unalijua fika.

Gharama ya kutokuwepo kwa amani huwa kubwa katika jamii yoyote ile. Kwa ufupi, haiwezi kukadirika. Wengi hulemazwa huku wengine wakipoteza roho zao. Mali yaliyochumwa kwa muda mrefu huharibiwa kwa muda wa fumba fumbua. Mabilioni ya pesa huharibiwa kwa muda wa bata kutikisa mkia wake. Katika maeneo kama haya, wawekezaji hutoweka jambo ambalo huwanyima vijana nafasi za kujiendeleza. Maeneo kama haya huselelea nyuma kiuchumi.

Ni vizuri tuelewe kuwa dhima ya kulinda amani haiwezi kuachiwa asasi za kiusalama pekee. Lazima tushikane mikono kupigana na hali yoyote inayotishia usalama wetu kwa hali na mali. Taasisi za kielimu na kidini ziwe katika mstari wa mbele kuhubiri amani. Wanaotumia madhabahu kuwagawanya watu kwa misingi ya kidini watengwe na kukashifiwa. Viongozi wa kijamii nao wachangie kupiga vita mila potovu kama vile wizi wa mifugo na uvamizi. Wanasiasa wachochezi watemwe wakati wa uchaguzi.. Vijana nao wajiunge na vilabu vya kuhubiri amani nchini. Haya yakifanyika **dunia itakuwa paradiso yenye raha mustarehe.**

**31.** Kulingana na aya ya kwanza
- A. amani huimarishwa zaidi baada ya maelewano
- B. amani huweza kupatikana hata palipo na ugomvi
- C. kuwepo kwa amani huwawezesha watu kujifunza mengi.
- D. kwenye amani gharama ya vita hupungua

**32.** Kwa mujibu wa aya ya pili ni nini maana ya kauli hii?

'*Kama hujui kufa tazama kaburi.*'
- A. Iwapo hujawahi kuyaelewa matatizo chunguza chanzo chake.
- B. Endapo hukielewi kifo chunguza matokeo yake
- C. Iwapo hujawahi kukielewa kifo chunguza matokeo yake
- D. Kama hulielewi jambo, chunguza matokeo yake.

**33.** Chagua jibu sahihi kulingana na aya ya tatu.
- A. Amani ni hali ya utulivu palipo na vita
- B. Watu wengine hupuuza thamani ya amani
- C. Ukiingia gizani utajua umuhimu wa amani.
- D. Gharama ya amani huwa kubwa sana.

**34.** Kulingana na kifungu hiki, ni wazi kuwa
- A. lazima msimulizi anajua umuhimu wa amani
- B. visa vya utovu wa amani hutokea karibu na watu
- C. amani huweza kuvurugwa na matendo tusiyoyatilia maanani.
- D. amani yetu huvurugwa na wale tunaowazia kwa undani.



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi **| Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

35. Kifungu hiki kinapinga uenezaji wa uvumi kwa kuwa uvumi;
A. humwumiza mtu kihisia na kumfanya akose utulivu wa moyo.
B. una uwezo wa kutenga marafiki zake na hivyo kuwaumiza kihisia
C. una uwezo wa kumwumiza mtu kihisia na kumwongezea utulivu wa moyo
D. pengine una uwezo wa kumfanya mtu akose kujiheshimu

36. Ni nini maana ya **'yasipothibitiwa'** kulingana na kifungu?
A. Yasipoondolewa
B. Yasipozuiliwa
C. Yasipowezekana
D. Yasipopunguzwa

37. Wananchi katika kifungu wamelaumiwa kwa
A. kutowajua wanaotekeleza vitendo vya kihalifu
B. kuwaonya wenzao wanapotaka kutoa ushahidi wao
C. kuwafichua washukiwa wanaotafutwa na serikali
D. kukosa kuisaidia serikali katika kuwahakikishia usalama wao.

38. Kulingana na kifungu ulichosoma, mbinu mwafaka zaidi kukabiliana na wanasiasa wanaoeneza chuki katika jamii ni
A. kusambaza habari kuwahusu katika vyombo vya habari
B. kuwaondoa uongozini wakati wa kufanya maamuzi ya uchaguzi.
C. kuwatia mbaroni na kuwanyamazisha kabisa
D. kuwaacha wapige domo kwa kuwa hakuna marefu yasiyokuwa na ncha

39. Wazo kuu linalojitokeza katika aya ya mwisho ni kuwa
A. mila potovu ndizo zinazovuruga amani ya mwananchi wa taifa letu tukufu
B. asasi za kijamii hazihusiki katika kudumisha amani humu nchini.
C. jukumu la kulinda amani ni la kila mmoja wetu
D. tukishirikiana katika vita amani ya kudumu itapatikana.

40. Taja tamathali mbili zinazojitokeza katika kauli hii-:
**Dunia itakuwa paradiso yenye raha mustarehe.**
A. Chuku, kielezi cha kutilia mkazo
B. Nahau, kinaya
C. Ishara, tashbihi
D. Istiara, takriri

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 mpaka 50***

Mwalimu ni nani? Nina uhakika wa mauti kuwa umewahi kusikia neno 'Mwalimu' likitajwa. Huenda ukaniambia kwamba mwalimu ni yule ambaye anakufundisha masomo mbali mbali darasani. Kuna wale wengine huenda waseme kwamba mwalimu ni mtu ambaye anawarithisha wengine kimaarifa; yawe ya darasani au nje ya darasa. Almuradi kila binadamu anaweza kutoa maana anuwai za jina 'mwalimu' na namna mwalimu alivyomwathiri.

Kwa maoni yangu mwalimu ni mtu yeyote mwenye ujuzi ambaye anapitisha ujuzi huo kwa mtu mwingine mwenye kiwango cha chini cha ujuzi. Kuna uwezekano hata mwanafunzi ni mwalimu na mwanafunzi mwenzake. Hili nasema kutokana na Potosha mwanafunzi wa darasa la nane alikuwa mwalimu wa yote mabaya. Kila wakati mwanafunzi angepatikana katika hatia, alidai kuwa alishinikizwa na potosha. **Wengi walitahadharishwa dhidi ya kujinasibisha na potosha kwa kuwa wangeishia kutapakazwa sifa mbaya.**



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi **| Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

Nakumbuka ulikuwa muhula wa pili Jane aliingia akiwa msichana mwenye haya limbukeni. Rafiki yake wa kwanza akawapotosha. Potosha naye akamfunza mengi mawi.Baada ya muda mfupi Jane akawa tofauti kabisa. Akafuata yote ya **'mwalimu'** wake Potosha. Jane alikuwa msichana mrembo kupindukia. Lakini kutokana na mafunzo ya mwalimu wake Potosha, aligeuka na kuwa haambiliki wala kusemezeka. Akaingiwa na tamaa isiyo na kifani.

Usisahau haya yote yakiendelea walimu na wavyele wao walimfunza Jane umuhimu wa kuwa na maadili. Isitoshe, alifunzwa masomo vyema lakini akili yake ilikuwa butu. Kutokana na kupotoshwa na Potosha, Jane akawa haingizi chochote cha maana ila uchafu wa rafiki yake Potosha. Nyumbani nako hakuzingatia maonyo. Alikuwa kiguu na njia.

Wakati fulani wa sikukuu ya Pasaka, Jane alipomaliza tu shule ya msingi, alikutana na mwanaume mmoja, kipenzi cha wasichana wengi, mtajika kwa mali na umbo. Jino la mwanaume huyu aliyendwa na Jane lilikuwa likionana na jua.

Baada ya muda mfupi, Jane alijikuta akiwalea watoto wengine watatu wake mwenyewe. Ajabu ni kuwa, <u>**hilo halikumfanya Ghiliba kufumba jicho lake la nje**</u>. Alimarisha nyendo zake kiguu na njia, alipochoka, akaingia garini na kuikata mitaa. Jane aende wapi? Alifungika nyumbani ndi. Akamlea mwana huyu na yule, wake na wale wa kambo. Vijisenesesene na vikaongezeka. Lakini akajaribu kuvumilia akidhani kuwa angezila mbivu, lakini wapi? Alipoligema ilibidi alinywe. Siku zikaja na kupita.
Jane akajuta kuwa kutosikiliza wakuu na kukimbilia mtu ambaye hata hakuwa akimwelewa vizuri. Kwao nako kukawa hakuridhiki. Jane akajuta kuwa kutosikiliza wakuu na kukimbilia mtu ambaye hata hakuwa akimwelewa vizuri. Pesa na raha alizokuwa amezikimbilia akawa anasikisikia kama hadithi ndotoni. Kwao kukawa hakuridhiki. Jane akawa mjamzito tena, kama kawaida akaenda kliniki za wajawazito. Alipopimwa ikabainika kwamba alikuwa ameambukizwa ugonjwa wa zinaa lisilo na tiba. Mwana alipozaliwa akaaga. Ghiliba naye badala ya kumliwaza akawa wa kumzidishia mzigo kwa kumnyanyasa.

Baada ya humusi moja ya mwongo mmoja, tumbo na umbo la Ghiliba likaanza kutoweka. homa za hapa na pale, vipele, mara kukohoa, kuendesha, yote yakamvamia bila kumpa nafasi. Akamsingizia Jane kuwa ndiye aliyeleta maradhi. Waliokuwa pembe za chaki walijua ukweli ulipokuwa. Baadhi ya vipusa wake wakaanza kupukutika kama majani msimu wa mpukutiko. Pesa zikawaishia. Ghiliba na Jane hata wakashindwa kutimiza mahitaji muhimu ya kutunza siha zao. Ghiliba akawa wa kuingia na kutoka hospitalini naye Jane akawa anaviuguza vidonda ndugu vyake na vya mumewe. Hatimaye mumewe akabwagwa chini na akawaacha mkono.

Hakuna aliyemwelewa Jane. Walimwona kama pweza aliyejipalia makaa makubwa ya moto mkali. Karo ya shule ikawa ni shida. Huruma ikawaingia wote wa karibu na wa mbali. Wakasema lisilo budi hubidi na likibidi hutendwa. Wakabeba mzigo kwa hiari yao. Wakawafanyia watoto mchango wa karo na ada za matibabu. Mwishowe Jane akaungana na mumewe akiwa bado mbichi wa umri. Hata miaka ishirini alikuwa bado hajafikisha. ikabidi watoto walelewe na wahisani.

Kutokana na masaibu yaliyomsibu Jane, jamii ikaazimia kuwa wao hawangekuwa watumwa wa tabia iletayo ugonjwa wa ukimwi. Walitambua kuwa ukongo huu unarudisha nyuma maendeleo na kuipakaza jamii mizigo isiyotarajiwa. Hapo tutakuwa tukijihadhari kabla ya hatari. Likawa funzo kwa kila mmoja kuwa tamaa huua na tamaa nyingi mbele kiza.



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi **| Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

**41.** Kulingana na aya ya kwanza,
A. msimulizi anajua kuwa msemaji anafikiria kwa undani kuhusu mwalimu wake
B. neno 'mwalimu' lina maana tofauti tofauti kulingana na wahusika
C. mwalimu anapofundisha maarifa darasani watu wengi huyapitisha kwa wengine.
D. Akili inapojiwa na neno, "mwalimu," hurejelea maarifa ya nje.

**42.** Aya ya pili kulingana na kifungu inaonyesha,
A. watu wenye kiwango cha chini cha ujuzi hawajui maana ya elimu
B. shughuli za mwanafunzi darasani ni njia ya kupitisha maarifa kwa wengine
C. mwanafunzi anapofungia maadili ya wengi huishia kuwaelimisha wengi
D. wakati wadogo wanaposoma wanajua kwamba hawawezi kuwafundisha wakuu wao.

**43.** Ni methali gani mwafaka kuelezea ujumbe ulio katika kauli hii?
**Wengi walitahadharishwa dhidi ya kujinasibisha na potosha kwa kuwa wangeishia kutapakazwa sifa mbaya.**
A. Mchezea chuma huchuma, kama hakuchuma tumbo hunguruma.
B. Wengi wape usipowapa watanyakua
C. Tahadhari kabla ya hatari
D. Mchezea mavi hayaachi kumnuka

**44.** Jane alipoolewa na Ghiliba,
A. alikuwa amepata watoto nje ya ndoa
B. alikuwa ameshajua tabia halisi ya mumewe
C. alijiona bora kuliko watangulizi wake
D. aliamua kuwataliki wake wa awali

**45.** Jane aligundua vipi kuwa alikuwa muwele wa gonjwa lisilo na tiba?
A. Mwanawe alipoaga dunia akiwa hospitalini
B. Alianza kuugua maradhi mbalimbali kutoka kwa mumewe Ghiliba
C. Alipimwa katika kliniki ya wajawazito
D. Ghiliba mumewe alianza kudhoofika kiafya

**46.** **'Baadhi ya vipusa wake wakaanza kupukutika kama majani msimu wa mpukutiko.'** maana ya kauli hii ni kuwa
A. kuna marafiki wa Jane walianza kuaga dunia
B. baadhi ya marafiki wa Ghiliba walianza kufunga safari isiyo na marejeo
C. waliokuwa marafiki wa Jane na Ghiliba walianza kujitenga
D. wasichana warembo wa kijiji walianza kuugua mmoja mmoja

**47.** Jamii ya kifungu inajaliana masilahi sana maadamu
A. inawahudumia mayatima kwa njia ifaayo
B. inawaona wenzetu kama pweza wanaojiingiza katika taabu.
C. matoa michango kwa wanaougua ugonjwa wa ukimwi
D. inahamasisha watoto kuhusu maradhi ya ukimwi

**48.** "Kulingana na kifungu, ugonjwa wa ukimwi unasambazwa **zaidi** na
A. waume matajiri, wasichana walio chini ya umri
B. watu wasio na elimu, wanaume wenye wake wengi
C. kutowajibika kwa vijana , watu wasio waaminifu katika ndoa
D. watu wasiotulia nyumbani, wasichana warembo

**49.** Gonjwa la zinaa. Lipi si gonjwa la zinaa?
A. Ukimwi B. Kisonono
C. Kaswende D. Pumu

**50.** Ni nini maana ya , **'hilo halikumfanya Ghiliba kufumba jicho lake la nje.**
A. Ghiliba hakuacha kuwa na uhusiano nje ya ndoa
B. Ghiliba hakuacha shughuli zake za nje
C. Ghiliba hakuacha kuwapenda watu waliokuwa marafiki za mkewe
D. Ghiliba hakukoma kutafuta mali nje ya ndoa